**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE**
**SHULE YA SEKONDARI BUGENE**


**Namba za simu: 0734 88 88 95**
**Mkuu wa Shule: 0784 72 10 50**
**Makamu Mkuu wa Shule 0744 62 48 67 / 0753 44 38 22**
**Matron : 0765 16 90 39**
**Patron: 0755 41 28 48 / 0764 891394**
E-mail:bugeneseco@gmail.comn

Ofisi ya Mkuu wa Shule,

Shule ya Sekondari Bugene,

48 Mtaa wa John Pombe Magufuli,

S.L.P 198,
35404 Bugene,
**KARAGWE.**


Tarehe 12/06/2023

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi.................................
...................................................................
S.L.P..........................................................

**YAH:- MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUGENE HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE MKOA WA KAGERA MWAKA 2023/2024**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2023/2024 Tahasusi ya ..................Shule ya Sekondari Bugene ipo umbali wa Kilometa 8 kusini mwa mji wa Kayanga. Usafiri wa basi kutoka mjini Kayanga unapatika katika kituo cha mabasi Daladala nauli ni shilingi 1000/=, kwa wanaotokea mikoani unashukia kituo cha mwisho kabisa cha mabasi **Omurushaka.** Kutoka Omurushaka mpaka shuleni kwa usafiri wa Pikipiki nauri ni Tsh.1,000/=.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **14/08/2023** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/08/2023.**



CamScanner

**2. Michango kwa ajili ya uendeshaji wa shule.**

a) **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni Tshs 80,000/= kwa ajili ya uendeshaji wa shule.** Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule **Na. 31901100037** katika Benki ya **NMB** tawi la **KAYANGA (Unaweza kufanya malipo katika tawi lolote la NMB nchini).** Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye Pay in Slip).

**ANGALIZO**:- Jumla ya michango kwa wanafunzi wa bweni ni shilingi 80,000/=kwa mwaka.

**b) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

## 3.0 SARE YA SHULE

### 3.1 WAVULANA:-

i) Suruali mbili rangi ya Kahawia iliyokaza (Brawn) zenye urefu wa kufunika kisigino pasipo kuikanyaga, zisiwe nyembamba sana au pana sana upana wa inchi 18-20 miguuni unafaa (**Suruali za Modo hazitakiwi**). Suruali ziwe za kushona na kitambaa kiwe kizito.Suruali itapimwa kuthibitisha vipimo.

ii) Shati mbili nyeupe za mikono mirefu aina ya Tetroni, zenye mfuko mmoja upande wa kushoto.

iii) Mkanda mweusi wa ngozi upana usiozidi inchi mbili.

iv) Jozi za Viatu vyeusi vya ngozi pair 2 , visiwe mabuti na visigino vyake viwe vifupi. vyenye kufungwa kwa uzi.

v) Soksi nyeusi jozi mbili.Tai moja aina ya Pundamilia ya michilizi mweupe na Bluu.

vi) T-sharts 2 nyekundu za kushidia.

vii) Suruali 2 nyeusi za kushindia vipimo vilevile vva suali ya Kahawia iliyokaza.

### 3.2 WASICHANA:-

i) Sketi mbili rangi ya kahawia iliyokaza (Brawn) za rinda moja kubwa mbele na rinda jingine kubwa nyuma pembeni marinda madogo matatu pande zote mbili (**Mshono wa masisita**),usipo elewa mshono njoo utashonea huku kuna mafundi jirani na shuleni, upana wa mkanda usiozidi inchi mbili. Sketi iwe na urefu wa kutosha inchi sita chini ya magoti, kiwe kitambaa kizito.

ii) Shati mbili nyeupe za mikono mirefu aina ya tetroni. Blauzi iwe na mfuko mmoja upande wa kushoto. Tai moja aina ya Pundamilia ya michilizi mweupe na Bluu.

iii) Jozi za viatu vyeusi vya ngozi pair 2 vya kufunika na vyenye uzi visiwe mabuti na viwe na visigino vifupi.



CamScanner

iv) Soksi nyeupe jozi mbili.

v) Panjabi nyeupe pana 2 na Panjabi ana 1 ya njano(rangi ya chungwa) zinazofika chini ya magoti na jarabibi nyeupe mbili(2) **(Hii ni kwa waislamu wa kike tu).**

vi) Nywele kichwani zisizidi sentimeta moja.
vii) Gauni mbili 02 rangi ya bluu ya kushindia.

**3.3. SARE KWA WOTE:**

- Sweta ya shule Rangi ya Kijivu.
- Tsheti nzito rangi ya njano yenye Kora.
- Nywele fupi zisizozidi sentimeta moja, Kusuka, kuweka dawa ya nywele au kunyoa Kipara haviruhusiwi, Hairuhusiwi pia kubadili rangi ya ngozi na kucha. Bangili, Heleni, Pete, na vitu vingine haviruhusiwi shuleni.

**4.0 Nguo za Michezo:**

Aje na Track suiti Rangi ya Kijivu na viatu vya raba.

4.1 **VIFAA VYA KITAALUMA**

Unatakiwa uje na vifaa vya kutosha katika shughuli za masomo darasani:-

- Kalamu za wino na za risasi za kutosha.
- Kasha la vifaa vya hesabu.(Mathematical set)
- Rula.
- Madaftari makubwa (Counter Books 12-Quire 3).
- Kamusi ya Kiingereza (Oxford Advanced Learner's Dictionary).
- Rimu moja ya Karatasi ( aina ya **Photocopy Papers $A_4$ multifucional na. 1**) kwa kila muhula.
- File moja la kawaida kwa ajili ya kutunza mitihani yako.
- Scientific Calculator (kwa wanaosoma tahasusi ya CBG,HGE,HGL na HGK).
- Dissecting Kit kwa mwanafunzi wa Biologia tu.
- Vitabu vya masomo la Tahasusi uliyochaguliwa kusoma, kwa somo la GEOGRAFIA vitabu vinavyohitajika ni:- Physical Geography (Msabila) Human and Economic Geography practical (Zists Kamili).
- Kwa somo la BIOLOJIA aje na vitabu vya TIE for advanced level secondary school. Form V &VI.
- Kwa somo la KISWAHILI aje na vitabu vya (TIE) Kiswahili kidato cha V&VI Lugha na Sarufi na Fasihi.
- Kwa somo la HISTORIA aje na vitabu vya (TIE) History for advanced level secondary school form V.
- Kwa somo la ENGLISH LANGUAGE aje na Vitabu vya English for advanced secondary school form V(TIE).
- Kwa somo la ECONOMICS aje vitabu vya Microeconomics for advanced Secondary school,(TIE).Macroeconomics for advanced Secondary school(TIE).
- Kwa somo la CHEMISTRY aje na vitabu vya Organic Chemistry for advanced level secondary school(TIE) na General Chemistry advanced level secondary school (TIE).
- Kwa somo la MATHEMATICS aje na Basic Applied mathematics (TIE).



CamScanner

## 4.2 VIFAA VYA KAZI:

Unatakiwa kuja na vifaa vya kazi kwa ajili ya kutunza mazingira na shughuli za uzalishaji malia mbavyo ni:- Ndoo 2 ndogo(lita kumi) za plastiki zenye mifuniko, Siko 1,Jembe 1 Reki 1 mifagio 2 wa ndani na nje.

## 4.3 MALAZI

Shuka jozi 2 rangi ya bluu bahari, Godoro 2½' x 6', blanketi 1, mto 1, Foronya 2 bluu bahari,taulo 1 , Chandarua 1 nyeupe, Khanga jozi 1 maua ya bluu (kwa wasichana) na nguo za kulalia zisizobana.

## 4.4 MAHITAJI MENGINE

i) Kandambili jozi 1 za kuogea.
ii) Sabuni ya kufulia miche 5 (Kwa muhula).
iii) Sabuni za kuoga za kutosha.
iv) Mswaki/Miswaki na dawa ya meno.
v) Brashi ya kung'arisha viatu.
vi) Dawa ya viatu (ya kutosha).
vii) Toilet paper 5 (kila muhula).
viii) Tochi na betri zake (kwa tahadhari).
ix) Viatu wazi (Open Shoes) vya kushindia visiwe na visigino virefu.
x) Mafuta ya kujipakaa ya mgando (siyo vipodozi wala Lotion).
xi) Pedi pakiti 5 n.k (kwa wasichana) kwa muhula.
xii) Nguo za ndani za kutosha (Kwa wote).
xiii) Kikombe kimoja cha aluminium, Sahani ya aluminium na kijiko.

## 4.5 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Kama atapokelewa itabidi afuate sheria za shule na sheria za kuishi bweni ambazo ni pamoja na :-

i) Heshima kwa viongozi,Wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Preparation).
v) Kuwahi katika shughuli za shule utakazopewa.
vi) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mpaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vii) Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule.
viii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
ix) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
x) Kutunza mali za shule.
xi) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari .
xii) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini bila kuwajulisha wazazi wake,aidha kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie Ibada kwa siku na muda wa ibada ya dini yake(Wanafunzi wote ambao dini zao hazijaweka utaratibu mzuri wa ibada msikitini au kanisani wataabudia shuleni.
xiii) Mwanafunzi haruhusiwi kutumia mishumaa, taa ya chemli au kibatali bwenini na shuleni kwa ujumla.
xiv)) Mwanafunzi hutaruhusiwa kuletewa au kuleta aina yoyote ya chakula kwenye mazingira ya shule. Na kutunza bwenini.
xv) Ni marufuku, kunyoosha nguo ndani ya bweni wala darasani (Kunyoosha sare za shule kutafanyika nje ya bweni -Mf. Bwaloni au sehemu iliyotengwa kwa kazi hiyo kwa pasi ya mkaa.
xvi) Kila mwanafunzi ataleta sanduku kubwa la kutosha la mbao au la chuma ili kuhifadhi mali zake hawaruhusiwi kuwa na masanduku 2.
xvii)) Mwanafunzi akiugua zaidi ya uwezo wa shule kumhudumia, Shule itafanya mawasiliano na mzazi/mlezi wake kwa ajili ya matibabu zaidi kwa kutumia simu ya shule.
xviii) Kwenda nyumbani mara tu shule inapofungwa ndani ya vazi rasmi la shule/sare.



CS CamScanner

*MUHIMU:*

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa . Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumiwa na mwanafunzi mmoja tu:**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule kwa Msiba au Ugonjwa.**

**5. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i) Wizi.
ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote.
vi) Kusuka nywele . Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii) Kufuga ndevu.
viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix) Uvutaji wa sigara.
x) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi.
xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
xiv) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule. Endapo kuna lazima mwanafunzi kuwasiliana watatumia simu ya shule tu.
xvi) Kudharau Bendera ya Taifa.
xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
xix) Kukutwa nje ya uzio wa shule bila ruhusa.
xx) Kutokuheshimu na kutoshiriki kuimba nyimbo za Taifa.
xxi) Kuishi nyumba za kupanga(Ghetto)

**6. Viambatisho na Fomu Muhimu**

a) Fomu ya Uchunguzi wa afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali Hospitali binafsi haikubaliwi
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne, (4) za wazazi/walezi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.(Hakikisha pia unatupatia simu yenye huduma ya whatsap kwa ajili ya taarifa mbalimbali za kitaaluma).

**NB:- Kila Mwanafunzi anaagizwa kuja na kadi ya Bima ya Afya au Tsh 6000/= kwa ajili ya Bima ya Afya ya jamii (CHIF).Hautapokelewa bila kutimiza mojawapo ya Bina hizi.**



CamScanner

## MAMBO MENGINE MUHIMU YA KUFANYA KABLA YA KURIPOTI SHULENI

Unashauriwa kukamilisha na kuleta vitambulisho au utambulisho wa vitu vifuatavyo:-

i)**Vyeti / Cheti cha Afya:**
Lazima upimwe katika Hospitali ya Serikali na kujaziwa vipengele vya Afya yako na Daktari anayehusika katika fomu iliyoambatanishwa hapo

ii)**Cheti cha Uraia:**
Unatakiwa kuleta Shuleni hati ya Uthibitisho wa Uraia toka kwa Mkuu wa Wilaya yako au cheti cha kuzaliwa ( Birth Certificate) cha Serikali

iii)**Fomu za Utambulisho:**
Fomu maalum zimeambatanishwa. Ujaze fomu hizi kwa uangalifu na kisha unapokuja Shuleni kuripoti uziwasilishe.

iv) Cheti cha kuhitimu kidato cha nne.-Result Slip na Leaving Certificate.

v)**Sheria za Shule:**

Nakutumia Sheria za Shule ili uzisome na kuzielewa ili ufikapo shuleni upate kuzitekeleza ndipo utafanikiwa katika masomo yako. Baada ya kuzisoma weka **SAINI KUKIRI** ahadi ya kuzitekeleza na wazazi wako waweke sahihi kama mashahidi wako wa kukusaidia kutimiza sheria hizo kwa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai, kisha irudishwe shuleni. Unashauriwa kutoa nakala (Photocopy) kwa ajili ya Kumbukumbu wewe na Mzazi / Mlezi wako)

7. **Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

Saini ya Mkuu wa Shule ……Rwazo……

Jina la Mkuu wa Shule…LEONARD. B. RWAZO…

Mhuri wa Mkuu wa Shule………………………..

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI BUGENE
S. L. P 198,
KARAGWE, KAGERA

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli(wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:-**

Mkuu wa shule **0784 72 10 50, 0620563657**
Makamu Mkuu wa Shule **0744 62 48 67,0753443822**
Mwandamizi Taaluma **0621984812**
Mwandamizi /Malezi **0684589343,0769027221**



CamScanner

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. *JINA* KAMILI………………………………………………………………………………
**( *Jaza ilivyo kwenye* SELFORM)**
2. ANUANI YA NYUMBANI…………………………………………………………………
TAREHE YA KUZALIWA:…………………………………………………………………

3. MAHALI ULIPOZALIWA: MKOA…………………..WILAYA……………………..TARAFA……………
KATA:……………………… KIJIJI/MTAA…………………………………
4. ULIPOTOKA
SHULE YA MSINGI:…………………………..SEKONDARI……………………
ANUANI:………………………………………………………………………………….
5. DINI YAKO:…………………………..TAIFA *MTANZANIA/ SI MTANZANIA.
**(Futa lisilo sahihi)**

6. JAMAA KATIKA FAMILIA YAKO
(A) JINA LA BABA…………………………………………………………………………
ANUANI:……………………………………….NAMBA YA SIMU………………
ANAISHI/HAISHI KAZI YAKE………………………………………………………
(B) JINA LA MAMA………………………………………………………………………...
ANUANI………………………………………NAMBA YA SIMU…………………
ANAISHI/HAISHI KAZI YAKE:……………………………………………………...
(C) JINA LA MLEZI…………………………………………………………………………
ANUANI:……………………………NAMBA YAKE YA SIMU………………
ANAISHI/HAISHI KAZI YAKE:……………………………………………………..
UHUSIANO WAKE NA WEWE:……………………………………………………
(D) IDADI YA KAKA ZAKO:……………………………………………………………
(E) IDADI YA DADA ZAKO:……………………………………………………………
(F) WEWE NI MTOTO WA NGAPI KATIKA FAMILIA?..............................................
MIMI ……………………………..(Mzazi/Mlezi) wa mwanafunzi…………………………

**NIMEHAKIKISHA KUWA TAARIFA ZILIZOTAJWA HAPO JUU NI ZA KWELI AHADI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE NA KULIPA ADA**

Nimezisoma sheria/ kanuni hizi na kuzielewa na nitazitimiza/sitazitimiza kikamilifu.

JINA LA MWANAFUNZI:-………………………………………………………………

SAINI YA MWANAFUNZI:-……………………………….TAREHE…………………

JINA LA MZAZI/MLEZI………………………………………………………………

SAINI YA MZAZI/MLEZI:…………………………….TAREHE……………

**BUGENE SECONDARY SCHOOL**



CamScanner

## STUDENT'S MEDICAL EXAMINATION REPORT

1. STUDENT'S NAME……………………………………………………………
2. AGE:…………………HEIGHT(CM)…………WEIGHT(KG)……………
3. BLOOD EXAMINATION: HAEMOGLOBI………………………………

   : BLOOD GROUP………………………………

4. ANY ABNORMALITIES OBSERVED:…………………………………
5. STOOL EXAMINATION:…………………………………………………
6. URINALYSIS:…………………………………………………………
7. TB TEST (if negative was immunization given?)……………………………
9. CHEST :………………………………………………………………………
10. ANY COMPLAINT NOTED IN RELATION TO:-

   (a) ASTHMA………………………………………………………………

   (b) HEADACHE:…………………………………………………………

   (c)INABILITY TO EAT CERTAIN FOOD (MENTION THE REASON BEHIND)………

   (d) SKIN DESEASES:……………………………………………………

   (e) BILHARZIA (To be observed in distinguished clinics)…………………………

11. IS THERE ANYTHING ELSE TO BE KNOWN BY THE SCHOOL ADMINISTRATION……………………………………………………………………
12. ANY TREATMENT GIVEN………………………………………………………
13. DOCTOR/MEDICAL OFFICER RECOMMENDATIONS………………………………

   ……………………………………………………………………………………

NB: IN CASE ANY ONE OR SOME OF THE ABOVE REQUESTED EXAMINATION IS NOT UNDERGONE OR CARRIED OUT DO ANY RECOMMENDATION OR WRITE NAD FOR THE SAKE OF FUTURE CONVENIENCE.

14. DATE………………SIGNATURE OF EXAMINER……………………………………

DESIGNATION ……………………………………………………………………………

STATION

…………………………………………………………………………

OFFICIAL STAMP



CS CamScanner